

UHURU 24/02/2024 UK. 8

Simbachawene aitaka TASAF kulipa malimbikizo

Na ESTA MALIBICHE, Iringa

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameupa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) hadi Machi 5, mwaka huu, uwe umelipa malimbikizo yote yanayodaiwa na walengwa wa mpango huo nchini kote

Simbachawene alisema hayo jana katika ziara ya kutembelea wanufaika wa mpango huo unaolenga kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya watu waishio katika mazingira magumu aliyoifanya katika vijiji vya Migori na Kinywang'anga katika Jimbo la Isimani mkoani Iringa.

"Uongozi wa pamoja umesaidia sana utekelezaji mzuri wa miradi hii ya TASAF. Lakini kuna kelele kubwa inayohusu ucheleweshaji wa malipo kwa walengwa, nasema tusimgombanishe Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na walengwa. Ni haki yao kulipwa fedha kwa wakati," alisema.

Waziri huyo aliwataka viongozi wa TASAF kutoa malipo kwa wakati na kusositiza serikali haiwezi kukubali na haitamwacha salama ye yeyote atakayekiuka maagizo hayo.

Alieleza mpango wa TASAF wa kupigiwa mfano kwa kuwa unalenga kuongeza kipato cha kaya na kuwekeza katika afya na elimu ya watoto, kuinua uchumi kwa kujengà uwezo katika utunzaji rasilimali na kutengeneza njia mbadala na endelevu za ajira.

Alisema kaya maskini zilizokosa fursa ya kusajiliwa katika awamu zilizopita zisubiri awamu inayofuata itakayohusisha pia kuziondoa katika mpango huo kaya ambazo maisha yake kuitia utekelezaji wa shughuli za mpango, maisha yao yameshakuwa nafuu na bora kuliko ilivyokuwa awali.

"Kipindi cha pili cha TASAF kililenga kuongeza kipato na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa walengwa na kulinda maslahi ya watoto wao. Tunaamini wapo wengi ambao mambo yao yamebadilika katika kipindi hicho ambao wanapaswa kutoka katika mpango kuruhusu wengine wenye maisha duni kuingia," alibainisha.

Simbachawene aliagiza TASAF katika awamu ijayo ya mpango huo kuwekeza nguvu zaidi katika kusajili kaya maskini zenye watu wenye ulemavu kuendelea kumpa faraja Rais Samia anayetaka kuona mpango huo unagusa makundi mengi zaidi yenye uhitaji.

MABADILIKO YA JINA

Aidha, Simbachawene alisema serikali inafikiria kubadili jina la mpango huo kutoka kuitwa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na kuwa Mpango wa Kuboresha Maisha ya Wananchi.

"TASAF ni uwekezaji mkubwa sana, ni mfano bora katika kuondoa umaskini, inashirikisha wananchi na ni uvezeshaji kiuchumi, ina miradi ya mfano na ya gharama nafuu inayogusa maisha ya mwananchi huku huduma zake zikiunganisha maskini na matajiri wazipate kwa pamoja, kwahiyio huko mbele ni muhimu tukabadi jina," alisema.

Awali, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Iringa, Venance Ntiyalundura alisema tangu kuanzishwa kwake, mpango huo umewezesha mkoa wa Iringa wenyewe zaidi ya walengwa 30,000 kupata sh. bilioni 16.8 ambazo kati yake, sh. bilioni 13 ni ruzuku kwa wanufaika, huku zinazobaki zikienda katika miradi inayotoa ajira za muda na kwa vikundi vyatukopa na kurejesha.